# NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO -MASWALA YA JAMII

## Kipindi cha tisa ”Siamini"

**Mwandishi**:Chrispin Mwakideu

**Mhariri**: Andrea Schmidt

**Wahusika**:
Eveline(19),Meya(50),Madiwani(30+),Beti(12),Roni(14),Mapito (40)

**Msimulizi:**

Hujambo na karibu katika kipindi chetu cha Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu maswala ya jamii – jinsi ya kuwa mshirika katika siasa. Katika kipindi kilichopita, Eveline Mapito alinyakua kiti cha udiwani cha Milimani akiwa na umri wa miaka kumi na tisa tu! Ingawa alishindana na wapinzani wakubwa, ushupavu na uaminifu wake uliivutia mioyo ya wapigaji kura. Babake, ambaye alipigwa risasi, bado yuko hospitalini baada ya kufanyiwa upasuaji. Karibu katika kisa cha leo kwa jina “Siamini”.

**<u>Onyesho la Kwanza: Mkahawa mmoja mitaani</u>**

**SFX: Sauti ya juu ya muziki na watu wakiongea**

**1.EVELINE:** Samahani.. Kimya! Kimya! (anaita) Hey tafadhalini naomba upunguze sauti ya muziki..

(**Sauti inapunguzwa lakini inasikika kwa mbali**)

Asante! Nilitaka tu kusema huu si ushindi wangu peke yangu, bali

wetu sote! Sote kwa pamoja tumefanikisha uchaguzi huu. Mara kwa mara tumeambiwa sisi vijana ndio viongozi wa kesho, lakini sikubaliani na msemo huo kwani sisi ndio viongozi wa leo! Shuleni tunafundishwa kwamba ngoja ngoja…

**2.UMATI:** Huumiza matumbo!

**3.EVELINE**: Kwa hivyo hatutangoja kuumia matumbo yetu..leo tumedhihirisha kwamba vijana wanaweza kuongoza..ninawaomba hasa wasichana wenzangu tujitoe muhanga katika mambo ya maendeleo ya vijana wote kwa jumla na wajihusishe na siasa nchini mwetu..

**SFX: Shangwe na Nderemo/Mbinja**

Hata kama huu ndio msimu wangu wa kwanza katika siasa kama diwani.. napenda kuwaeleza kuwa nitawatumikia nyote kwa moyo thabiti ili mupate huduma bora bila kujali kama ulinichagua au la…!!!

**MSIMULIZI**: Watu wengi huingilia siasa kwa ajili ya matumbo yao na tamaa ya kutajirika haraka. Lakini si kweli kwa diwani mpya wa Milimani. Ni aina mpya ya mwanasiasa ambaye baraza la mji halimzowea. Na huko nyumbani kwa Mapito….

**Muziki unsikika**

**<u>Onyesho la pili: Nyumbani kwa Mapito</u>**

**1.BETI**: ( **akiita**) Roni.. Roni.. Kuna barua ya kila mmoja hapa.. yako, yangu na Eveline.. haya toboa siri, ni nani huyo aliyekuandikia?

**2.RONNIE**:  Hebu usinianze.. hata sikumbuki ni lini nilipopokea

barua mara ya mwisho

**3.BETI**: Hiyo ni kwa sababu huwa hauandiki barua yoyote…daaah…

**4.RONNIE**: Wewe..Betty .. chunga mdomo wako hakuna wa kukutetea…

**5.BETI**: (**furaha**) Lakini si baba yuwaja mchana, kwanza hatujamaliza kumtayarishia chumba chake..

**SFX: Barua inasikika ikifunguliwa**

Tazama hata hujui kufungua barua.. utairarua (**amcheka**) Hahahaha!!!!

**6.RONNIE:** Nyamaza! pilipili usiyoila yakuashia nini? Fuata lako tafadhali.. (**baada ya kusoma anapiga nderemo kwa furaha**) Yeeeeah!!!! Beti nimefanikiwa….

**7.BETI:** Ingelikuwa wewe si kakangu ningelikuita kichaaa….

**8.RONNIE**: Sikiliza… Beti, (**kwa bashasha**) Kwa Roni Mapito.. ni furaha yetu kukujulisha kuwa wakufunzi wetu walivutiwa sana na uchezaji wako kwenye mechi ya fainali hivi kwamba tunakualika ujiunge na kikosi cha taifa cha wachezaji chini ya miaka kumi na sita kitakachoiwakilisha nchi hii katika safu za michezo ya kimataifa inayokuja…(**apiga usiyaa)** Yeeeeeeh!!!

**9.BETI**: Woooooow!!! Hiyo ni poa!!! Pongezi! lakini.. sielewi….si mulishindwa katika mechi hiyo?

**10.RONNIE**: Wewe ni msichana Betty, huelewi mambo haya! Ndoto yangu imetimia!!!

**11.BETI**: Imetosha bwana Ndoto!! Sasa ni zamu yangu.. na hivi ndivyo unavyofungua barua….

**SFX: Barua inafunguliwa/ Sauti ya karatasi**

Ooohhh!!! Hapana!!!! Haiwezekani.. Ooooohh!!!( **akilia kwa uchungu mwingi**)

**12.MSIMULIZI**: Kilio hicho bila shaka ni cha mshangao na madhila. Huku akitiririkwa na machozi, Beti hakuyaamini aliyokuwa akiyasoma ndani ya barua ile wakati akumueleza kake Roni. Wakati huo huo, baraza la mji wa Milimani linakutana kwa mara ya kwanza baada ya uchaguzi.

**<u>Onyseho latatu: Mkutano wa kwanza wa Madiwani</u>**

**1.MEYA:** Karibuni mabwana.. napenda kuwapongeza nyote kwa ushindi wenu..na kuwakaribisha nyote katika baraza la jiji letu. Pia ningependa kuwaalika kwa sherehe ya kufahamiana nyumbani kwangu…

**2.EVELINE**: Mheshimiwa meya wetu, nilisikitishwa sana ulipolisabahi baraza hili kama la wanaume pekee.. hata kama ndimi mke pekee hapa lakini ni muhimu nikitambuliwa uwepo wangu..Pili, utaniwia radhi kwani napenda kufahamiana nawe na madiwani wote nikiwa hapa ofisini na wala sio kwako nyumbani..

**SFX: Vicheko vya wanaume**

**3.MEYA:** Bila shaka wewe ni mgeni hapa.. sivyo?

**4.EVELINE**: Kwa majina ni Eveline Mapito, diwani mpya wa Milimani. Mimi ni mgeni katika baraza hili…
**5.MEYA**: Alaaaah! Kumbe ni wewe… kwa kweli sikutarajia

kukuona hapa.. Samahani sana kwa kutojua kwangu.. Ni mara ya kwanza mwanamke kuchaguliwa diwani, kwa hiyo kwa njia fulani umebadili desturi za baraza hili.. hata hivyo nakukaribisha uje katika sherehe yetu nyumbani kwangu....Kwa uzuri wako bila shaka utazidi kuing'arisha sherehe yetu ya mwaka huu..lakini tafadhali usibebe simu yako ya mkononi……

**SFX: Minung'uno  na vicheko vya kejeli vinasikika**

**6.EVELINE**: Nakubali kuwa mimi ndiye mwanamke pekee hapa, mdogo kiumri na nisiye na uzoefu, lakini kamwe sitokubali kuhujumiwa… nina maono na nia ya kuwasaidia watu wangu kwa hiyvo sitokuja shereheni bwana Meya… asante..

**SFX: Makofi hapa na pale**

**7.MEYA**: Hmm..umri wako?

**8.EVELINE**: Nitatimu miaka ishirini hivi punde..kwanini?

**9.MEYA**: Si nadhani ungefaa kuwa shule?

**10.EVELINE**: Kwa heshima zote.. Nikidhania hivyo kwako.. kwamba unahitaji kuwa umestaafu.. tangu nizaliwe umekuwa meya wa jiji hili sivyo?

**SFX: Madiwani wakizozana kwa sauti za manun'guniko**

**11.MEYA**: Kwa hivyo leo hii tayari umekuwa mkaidi? Wacha nikupe habari msichana wewe. Sisi ndio wenye baraza hili, bidii yangu ndio imeniweka kitini miaka yote hiyo, sawa?

**12.EVELINE**: Bwana meya .. sikuja hapa kutafuta maadui .. lakiniiiiii…..

**13.MEYA**: **(kwa hasira)** Baraza limeahirishwa!!!

**14.MSIMULIZI:** Eveline alikumbana na mapokezi ya chuki kutoka kwa meya wa mji wa Milimani na madiwani wenzake.. Nyumbani Mapito amejawa na huzuni aliporudi nyumbani na kukumkuta binti yake Betty akilia…

**Onyesho la nne : nyumbani kwa mapito**

**1.MAPITO:** Betty kula chakula kitapoa…

**2.BETI**: Sihisi njaa na wala hamu ya kula pia sina..

**3.MAPITO**: Usiwe na simanzi.. sote tunasikitika kwa nini wamechaguwa shule nyengine kwenda ikulu kumuimbia raisi wakati ni nyinyi mlioshinda ….lakini si neno Betty.. bado kuna nafasi ya ufanisi mkubwa katika simu za usoni……

**4.BETI**: (**akilia**) Sidhani kama kuna mafanikio mengine katika siku zijazo.... tulifanya mazoezi kwa bidii tukilenga kumuimbia raisi wetu.. kwa nini washindi kunyimwa haki yao???

**5.MAPITO**: Najua, najua.. hebu acha kulia.. Nimesoma katika barua yako kwamba mtapelekwa sehemu nyengine.. Si hyo ni afadhali kuliko kukosa kabisa?

**6.BETI**: La..(**kwa uchungu**) Wametuibia ushindi wetu.. Je nitawaeleza nini wenzangu katika kwaya?

**7.RONNIE**: Beti, tulia…wewe ni muimbaji mzuri na umeshinda. Hakuna anayeweza kuwapokonya sifa hiyo…
**8.BETI:** Ni rahisi kwako kusema hivyo….kwa vile wewe umechaguliwa kuchezea timu ya taifa…

**9.MAPITO**: Kwa nini usimuulize Eveline? Yeye ni diwani sasa.. Labda anaweza kulifuatilia swala hili katika wizara ya elimu…

**10.BETTY**: (**akitabasamu)** Naam hata nimesahau! Ndiyo Eveline .. Eveline atatusaidia bila shaka…

**11.MAPITO**: Amesharudi kutoka mkutano wa baraza la mji?

**12.RONNIE**: Bado hajarudi… nina hamu sana kujua mkutano huo ulikuwaje.

**13.MAPITO:** Sitamani kujua .. najua amepata dhiki kuwa katikati ya wanaume**…**

**14.BETI**: Baba wajua nini? Sasa hamu ya kula imerudi!

**15.MAPITO:** Haaaaah! Imerudi? Sawa, hivyo ni vizuri Wanangu… ninawafurahikia sana… sasa Roni unakutana lini na wenzako walio katika timu ya taifa?

**16.RONNIE**: Wiki ijayo, sijui itakuwaje na nitarajie nini… watu wananiambia mambo ni tofauti, sio kama timu ya shule…

**17**.**BETI**: Baba….

**18.MAPITO**: Naam msichana wangu.

**19.BETTY**: Twafurahi umerudi nyumbani...

**Mwisho wa kipindi cha Tisa**

**Msimulizi**:

Naam. Roni amechaguliwa kujiunga na timu ya kandanda ya

vijana wa chini ya umri wa miaka 16. Changamoto kubwa na ngumu inamsuburu. Je ataweza? Beti amevunjika moyo sana kwa habari kuhusu kwaya yake na Eveline naye anaona vigumu kuwa na marafiki katika mkutano wake wa kwanza wa baraza la mji. Ili kujua kitakachotokea, jiunge nasi tena wiki ijayo. Kumbuka msikilizaji unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kwenye mtandao. Tovuti yetu ni: www.dw-world.de/lbe